

Sixth Floor, Harbourview Towers, Samora Avenue
P O Box 72175, Dar es Salaam, Tanzania
TEL: (+255-22) 2123850; 2123853; 2123854; 2123856; FAX: (+255-22) 2123180
E-mail: info@ewura.go.tz Website: <http://www.ewura.go.tz>

KINAHITAJIKA KIWANJA

Tangazo la Zabuni

Tarehe 1.06.2009

1. Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imetenga fedha katika Bajeti yake ya mwaka wa fedha 2008/2009 ambapo sehemu ya fedha hizo itatumika kulipia gharama ya kiwanja cha kujenga Ofisi za kudumu za Mamlaka hiyo Jijini Dar es Salaam.
2. Eneo la kiwanja hicho liwe limepimwa na lenye ukubwa wa kati ya mita za mraba 3000 na 4000.
3. EWURA inakaribisha maombi ya zabuni kutoka kwa wananchi wenye nia ya kuiuzia Mamlaka kiwanja chenye sifa zilizotajwa hapo juu. Mzabuni atatakiwa kueleza bei na masharti ya uuzaji wa kiwanja husika.
4. Waombaji wa zabuni hiyo wanaweza kupata maelezo zaidi kutoka kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya EWURA, Mtaa wa Samora/Mission, Jengo la Harbour View Towers, Ghorofa ya Tano, Chumba Namba 516, S.L.P 72175, Dar es Salaam kuanzia saa 2:00 za asubuhi hadi saa 10:30 jioni kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za mapumziko.
5. Barua za kutaka kuuza kiwanja zilizo katika nakala halisi Moja (1) na nakala kivuli Tatu (3) zilizofungwa kwenye bahasha ziandikwe **"ZABUNI YA KUUZA KIWANJA"** na kuwasilishwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya EWURA, Mtaa wa Samora/Mission, Jengo la Harbour View Towers, Ghorofa ya Tano, Chumba Namba 516, S.L.P 72175, Dar es Salaam kabla ya Jumanne tarehe 30.06.2009 saa 8.00 mchana. Zabuni zitafunguliwa mbele ya waombaji au wawakilishi wao watakaopenda kuhudhuria ufunguzi huo siku na saa hiyo hiyo kwenye ukumbi wa mikutano wa EWURA uliopo Ghorofa ya Sita, Mtaa wa Samora/Mission, Jengo la Harbour View Towers.

MKURUGENZI MKUU

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI